



## Afasia ni tata ya lughha

Watu ambao wanaugua kutokana na afasia huwa na shida ya **kuongea, kuelewa, kusoma, kuandika na kufanya hesabu.**

**Chanzo** cha afasia kwa kawaida huwa **madhara ya ubongo**. Katika kesi nyingi hii huwa ni **kupindwa na mshipa**, lakini pia **ajali au kidonda** inaweza kusababisha afasia.



Mtu huugua kutokana na kupindwa na mshipa wakati **mzunguko wa damu** katika ubongo unatatizwa kwa **ghafla**.

Hii inaweza kutokana na mambo mawili: mshipa wa damu unaweza **kuzibika** au mshipa unaweza kuanza **kuvuja**

### Kuzibika:

Kwa ajili ya **kunenepa kwa ukuta wa mshipa** (thrombosis) au kwa maana ya **damu kuganda** (embolism) mshipa unaweza kuzibika.

Hii inaitwa *cerebral infarction*



### Kuvuja:

Sehemu **nyepesi** inaweza kuundika ndani ya mshipa (aneurysm); na sehemu hiyo inaweza **kupapa** na kuanza **kuvuja** au **kupasuka**.

Hii inaitwa *cerebral hemorrhage*



Madaktari kwa kawaida huiita kupindwa na mshipa CVA; **Cerebral Vascular Accident**



Lugha huwa na sehemu muhimu katika maisha yetu ya kila siku.

**Tunazungumza** na watu wengine, **tunasoma** magazeti, **tunafanya kazi** na **tunaelimika**.

Pia tunatumia lugha kutunga **fikira** zetu na kutoa **mipango** za siku za usoni.

Watu ambao wanaugua kutokana na afasia wanaweza kuwa na **shida** katika mambo kadhaa ambayo kabla ya afasia yalikuwa ya kawaida:

- Kuzungumza
- Kuongea na wenzio au katika mazingira yenyе kelele
- Kusoma kitabu, gazeti au jarida au hata alama za bara barani.
- Kuelewa na kusema vichekesho
- Kuelewa vipindi kwenye runinda au redio
- Kuandika barua au kujaza fomu
- Kupiga simu
- Kufanya hesabu, kukumbuka nambari au kukabiliana na pesa
- Kutaja jina zao au majina ya wanafamilia zao



Watu wanaougua kutokana afasia huwa na shida katika lugha, lakini **sio wenda wazimu!**

Watu wengi ambao wanaugua kutokana na afasia hupata kuwa maisha yao **yamebadilika** sana.

Mambo ambayo yalikuwa rahisi mwanzoni, yanachukua **muda na jitihada** nyingi.

Watu wengi ambao wanaugua kutokana na afasia **hutokuwa na udhabit** na kuwa na **kuhangai** kuhusu jinsi ya kuendelea na maisha.

**Msaada na himili** kutokana na mazingara yao ni muhimu sana.

Kukutana na watu wengine ambao wanaugua kutokana na afasia pia husaidia.

Watu wanaougua kutokana na afasia **huelewana bila kutumia maneno**.

Wewe unaweza kufanya nini?

- **Waambie watu** kuwa unaugua kutokana na afasia
- Vaa **cheti ndogo**, ambayo inaonyesha afasia ni nini
- Bainisha kile unachomaanisha kwa kutumia **gesture\***, **michoro**, **maandishi**, au **onyeshea kidole** kama kusema hakuendi vyema
- Omba **msaada** kwa familia
- **Tangulia kwa kupanga**, andaa gumzo kwenye fikira zako au kwenye karatasi.
- Gawa hangaiko zako na wengine; usihangaike peke yako.



gesture



michoro



maandishi



onyeshea kidole